Azimio La Kuangamiza Ukatili Dhidi ya Wanawake

Umoja wa Mataifa

Azimio A/RES/48/104 Lilikubaliwa tarehe 20 Desemba 1993

Baraza Kuu,

Kutambua umuhimu wa wanawake kutumia msimamo wa ulimwengu wa haki za wanawake kuhusu usawa, usalama, uhuru, uaminifu na heshima ya wanadamu wote.

Ifahamike kwamba haki na maazimio hayo yamehifadhiwa katika hati rasmi za kimataifa zikwemwo Azimio la Haki za Binadamu ulimwenguni, Mkataba wa kimataifa kuhusu Haki za raia za kisiasa, kisheria na kijamii, mkataba wa kimataifa wa haki za kiuchumi na asasi zote za kijamii, Mkataba wa kupiga marufuku ubaguzi wa aina yoyote dhidi ya wananwake na azimio dhidi ya ukatili na dhuluma zingine zozote zinazoshusha hadhi ya binadamu au kumwadhibu.

Kutambua utekelezaji mwafaka kuhusu kongamano la kuangamiza ubaguzi wa aina yoyote dhidi ya wanawake utachangia kuangamizwa kwa ukatili dhidi ya wanawake pia Azimio la kuangamiza ukatili dhidi ya wanawake lililoanzishwa katika mkataba huu litaimarisha na kuboresha mpango huo.

Kujali Ukatili dhidi ya wanawake kama pingamizi ya kupata mafanikio ya usawa, maendeleo na amani kama ilivyotambuliwa katika mikakato ya Nairobi ya Baadaye ya kuwafaa wanawake ambapo hatua za kupambana na ukatili dhidi ya wanawake zilipendekezwa na kutekelezwa kikamilifu kwa Azimio la uangamizaji wa hali zote za ubaguzi dhidi ya wanawake.

Kukiri kuwa ukatili dhidi ya wanawake ni sawa na kukiuka haki na msingi wa uhuru wa wanawake na kukatiza au kuingilia furaha ya haki na uhuru huo na kuhusu kukosa kutambua na kuimarisha haki na uhuru huo kwa muda mrefu hasa kuhusu ukatili dhidi ya wanawake.

Kutambua kuwa ukatili dhidi ya wanawake ni dhihirisho la kihistoria kuhusu kutokuwa sawa kwa uhusiano kati ya wanaume na wanawake ambao umesababisha wanawake kukaliwa na kubaguliwa na wanaume. ukatili dhidi ya wanawake ni chombo mahsusi kinachotumiwa na jamii ili kuwadhahilisha wanawake katika nafasi ya chini wakilinganishwa na wanaume.

Kujali makundi kadhaa ya wanawake kama wanawake wanaotoka kwenye makundi ya wachache,kina mama wa kiasili, wanawake wakimbizi, wanawake wanaoishi mashambani, wanawake maskini, wanawake walio jela au vizuizini, watote wa kike, wanawake walio na ulemavu, wanawake wakongwe na waliokumbwa na janga la vita, wote hao ni wenye kudhuriwa na ukatili.

Kumbuka makubaliano katika aya ya 23 ya Azimio la kiuchumi na halmashauri ya kijamii la 1990/15 tarehe 24 Mei 1990 ambalo lilitambua kwamba ukatili dhidi ya wanawake katika familia na jamii ni jambo laliloenea kote na kuathiri uchumi, matabaka na utamaduni hivyo basi hatua za haraka na kudumu lazima kuchukuliwa ili kuangamiza kuwepo kwake.

Kumbuka pia Azimio la kiuchumi na halmashauri ya kijamii la 1991/18 tarehe 30 Mei, 1991 ambapo baraza lilipendekeza kuanzishwa kwa mfumo Duniani utakaoweza kushughulikia kwa swala hili la ukatili dhidi ya wanawake.

Kufurahia jukumu la muungano wa kina mama la kutangaza na kuelimisha watu kuhusu ukubwa, uzito na asili ya shida hii ya Ukatili dhidi ya wanawake.

Mshtuko kwamba nafasi za wanawake za kuweza kupata usawa wa kisheria, kijamii, kisiasa na kiuchumi katika jamii umekuwa finyu kwa sababu ya kuongezeka kwa ukatili uliokithiri.

Imethibitika kwamba kulingana nay ale yaliyotajwa, kuna haja ya ufafanuzi mwafaka wa ukatili dhidi ya wanawake, kauli iliyo wazi kuhusu ya haki zinazoweza kutumiwa ili kuangamiza ukatili

wa aina yoyote dhidi ya wanawake. Serikali mbalimbali pia zithibitishe jukumu lao na kujitolea kwa mataifa ya ulimwengu kuangamiza ukatili dhidi ya wanawake.

Kutangaza Ahadi kwamba Azimio hili la kuangamiza ukatili dhidi ya wanawake litashughulikiwa vilivyo, kujulikana na kuheshimiwa.

KIFUNGU CHA 1

Kwa madhumuni ya Azimio hili kauli “Ukatilidhidi ya wanawake” ina maana ya kuwa ukatili wowote wa kijinsia unaosababisha au kutaka kusababisha madhara ya mwili, kimaumbile au kisaikolojia au kule kuleta shida kwa wanawakevikiwemo vitendo vya kushurutishwa kiholela hata kama vitatokea mbele za watu au kisiri.

KIFUNGU CHA 2

Ukatili dhidi ya wanawake waweza kueleweka kuwa unajumuisha mengi lakini si finyu kwa yafuatayo a) Ukatili wa mwili, kijinsia na kisaikolojia unaotokea katika familia ikiwemo kupigwa na kunajisiwa kwa watoto wa kike katika familia ukatili kwa sababu ya ulipaji mahari, ubakwaji katika ndoa, kukereketa sehemu nyeti na desturi zingine zozote zilizo na madhara kwa wanawake, ukatili usiosababishwa na mwenzi katika ndoa na ukatili unaohusiana na unyonyaji;

b) Ukatili wa mwili, kijinsia na kisaikolojia unaotekea katika jumuia ukiwemo unajisi, ubakaji, usumbufu na maonevu ya kijinsia na tishio kazini, katika taasisi za Elimu na popote pale wanawake wanapodhuhumiwa kwa kuuzwa na kulazimishwa kujihusisha katika biashara ya ukahaba;

c) Ukatili wa kimwili, kijinsia na kisaikolojia unaochangiwa au unaoungwa mkono na serikali

KIFUNGU CHA 3 Wanawake wana haki ya kufuruhia usawa na ulinzi, Haki za binadamu na uhuru wa kimsingi katika siasa, uchumi, kijamii, kitamaduni, kiraia au katika nyanja zingine zozote. Haki hizi zinahusu: a) Haki za kuishi b) Haki ya usawa c) Haki ya Uhuru na usalama wa binadamu d) Haki ya ulinzi chini ya sheria e) Haki ya kuwa huru na desturi zozote za ubaguzi. f) Haki ya kufikia upeo wa afya nzuri kimwili na kiakili g) Haki ya hali njema na adilifu kazini. h) Haki ya kutoteswa au kufanyiwa ukatili, unyama au vitendo vyovyote vya dhuluma au kudunisha.

KIFUNGU CHA 4 Mataifa yanapaswa kulaani ukatili dhidi ya wanawake na wasifuate mila, desturi au msimamo ya kidini ili waepukane na jukumu hili. Mataifa lazima yatafute mbinu za haraka na sera za kusaidia kumaliza ukatili dhidi ya wanawake na yafuatayo yashughulikiwe: a) Angalia pale ambapo haya hayajafanyika, kuidhinisha au kukubali azimio juu ya kumaliza ubaguzi wa aina yoyote dhidi ya wanawake au kuondoa shaka kuhusu azimio hilo; b) Kukoma kujihusisha na ukatili dhidi ya wanawake. c) Kushiriki kikamililifu ili kuzuia, kuchunguza na kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria zilizowekwa vitendovyote vya ukatili dhidi ya wanawake vilivyoanzishwa na taifa lolote lile au na mtu binafsi. d) Kutekeleza adhabu uraia, kazi na sheria zote za kinyumbani ili kuadhibu na kurekebisha makosa yote yaliyofanyiwa dhidi ya wanawake; Wanawake waliofanyiwa ukatili wapewe haki na ulinzi wa sheria kama ilivyokubaliwa katika sheria za ulimwengu, haki na suluhisho la kudumu; Mataifa yapaswa kuwafahamisha wanawake kuhusu haki zao wanapotafuta haki dhidi ya dhuluma walizotendewa; e) Angalia uwezekano wa kutekeleza mipango ya kitaifa ya kuimarisha usalama wa wanawake dhidi ya ukatili wa aina yoyote au kuweka mipango kabambe kwa madhumuni ya kuimarisha shughuli hiyo kwa kushirikisha mashirika yasiyo ya kiserikali hasa yale yanayoshughulikia swala hili la ukatili dhidi ya wanawake; f) Kutekeleza kwa njia pana mbinu zote za kuzuia ziwe za kisheria kisiasa na za kitawala, kitamaduni ili kuimarisha usalama ya wanawake dhidi ya Ukatili na kuona kwamba uonevu wa wanawake haufanyiki kwa sababu ya sheria zisizojali usawa wa kijinsia, unaoshurutisha au za uvamizi; g) Kufanya kazi na kuona kwamba kwa uwezekano wa rasilimali na msaada unapohitajika kulingana na kilimwengu, wanawake wanaofanyiwa ukatili na

inapowezekana watoto wao wapewe usaidizi maalum kama kawaida kuishi maisha ya kawaida, usaidizi wa ulezi wa watoto, matibabu, ushauri, matibabu na huduma kwa jamii, vifaa na mipango ya kuwasidia na kuchukua hatua zifaazo ili kulinda usalama wao na kuwasaidia kuishi maisha ya kawaida ya kimwili na kisaikolojia; h) Serikali zifanye makadirio ya pesa yatakayotosheleza shughuli za kuangamiza ukatili dhidi ya wanawake; i) Chukua hatua kuona kwamba maafisa wanaohusika na utekelezaji wa sheria na wale wa umma walio na wajibu wa kuona kuwa kuzuia, kuchunguza na kutoa adhabu dhidi ya ukatili kwa wanawake wamepewa mafunzo ya kuwahamisisha juu ya mahitaji ya wanawake; j) Kukubali hatua zote hasa katika nyanja ya Elimu ili kubadilisha mienendo ya kijamii na kitamaduni ya wanaume na wanawake na kuangamiza Ubaguzi, mienendo mibovu ya kimila na mingine mingi inayojikita kwenye fikira duni au za ukuu za kijinsia na wajibu wajiku wa jambo lisilo na uasili kwa wanaume na wanawake; k) Kuimarisha utafiti, kukusanya habari na kupanga takwimu hasa kuhusu ukatili wa kinyumbani ulioenea na ukatili wa ainanyingi dhidi ya wanawake na piakuhimiza utafiti kufanywa ili kujua sababu, chanzo, uzito na madhara ya ukatili dhidi ya wanawake na jinsi hatua zilizochukuliwa zinavyoathiri kuzuia na kurekebisha ukatili dhidi ya wanawake; Takwimu hizo na matokeo ya utafiti yatawekwa wazi kwa umma; l)Kubali hatua zinazolenga kuangamiza ukatili dhidi ya wanawake hasa wale wanaoweza kudhuriwa kwa ukatili; m) Kuwasilisha ripoti kufanyika kama inavyotakiwa kufanywa na mashirika yanayoshughlikia haki za binadamu ya Umoja wa Mataifa, habari kuhusu ukatili dhidi ya wanawake na hatua zilizochukuliwa ili kutekeleza Azimio la sasa; n) Kuhimiza kuimarishwa kwa mwongozo wa kusaidia utelekezaji wa hatua zilizopendekezwa kwenye Azimio hili. o) Kutambua umuhimu wa jukumu la muungano wa kina Mama na Mashirika yasiyo ya Kiserikali ulimwenguni ili kuunagana nayo kwa kuhamasisha watu na kuangamiza shida ya ukatili dhidi ya wanawake; p)Rahisisha na imarisha kazi ya muungano wa kina Mama na mashirika yasiyo na kiserikali na kushirikiana nayo katika ngazi za kinyumbani, kitaifa na kilimwengu; q) Himiza ushurikiano wa serikali mabalimbali za kimataifa zilizo wanachama ili zihusishe shughuli za kuangimiza ukatili dhidi ya wanawake katika mipango yao iwezekanavyo.

KIFUNGU CHA 5 Vyombo na mashirika maalum ya Umoja wa Mataifa yafaa yachangie katika kufahamika na kueleweka kwa haki na sheria zilizokubaliwa katika Azimio kulingana na nyanja zao mbalimbali kama ifuatavyo: a) Kuimarisha ushirikiano wa kimataifa na kiserikali kwa minajili ya kutambua mikakati ya kuangamiza ukatili, kubadilishana tajriba na kugharamia mipango inayohusiana na uuangamizaji wa ukatili dhidi ya wanawake; b) Kuimarisha mikutano na warsha kwa madhumuni ya kuunda na kuanzisha utambuzi kati ya watu juu ya swala hili la kuangamiza ukatili dhidi ya wanawake; c) Himiza ushirikiano na ubadilishanaji kulingana na mipango ya Umoja wa Mataifa kati ya mashiriko yanayoshughulikiwa kwa kina haki za binadamu hasa swala la ukatili dhidi ya wanawake; d) Kuhusisha uchunguzi uliotayarishwa an mashirika ya Umoja wa Mataifa kuhusu mifumo ya kijamii na tatizo kama yale ya ripoti za kipindi juu ya hali ya kijamii ulimwenguni, uchunguzi wa mwelekeo wa ukatili dhidi ya wanawake; e) Kuhumiza ushirikiano kati ya mashirika na yale ya Umoja wa Mataifa ili kujumuisha swala la ukatili dhidi ya wanawake katika mipango yao hasa kwa kuhisisha makundi ya Wnanwake wale wanaoweza kudhuriwa kwa ukatili; f) Kuimarisha utaratibu wa mwongozo au vitabu vya mwongozo vinavyohusiana an ukatili dhidi ya wanawake kwa kufuata hatua zilizopendekezwa kwenye Azimio la sasa; g) Angalia swala la kuangamiza ukatili dhidi ya wanawake kuwa muhimu katika kutekeleza mamlaka yao na kujali haki zao za kibinadamu; h) Shirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali katika kushughulikia swala hili la ukatili dhidi ya wanawake.

KIFUNGU CHA 6 Hakuna chochote katika Azimio hili kitakachoathiri hatua ifaayo ya kuangamiza ukatili dhidi ya wanawake ambayo itakuwepo kwenye sheria za taifa au katika Azimio lolote la kilimwengu, mkataba ama chombo chochote kinachotumiwa na Taifa.